# AGENDA ZA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO CHA MWEZI NOVEMBA, 2021 MNAMO TAREHE 17/12/2021

1. Kufungua Kikao

2. Kuridhia agenda za Kikao

3. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha tarehe 14/11/2021.

4. Yatokanayo na Muhtasari wa kikao cha tarehe 14/11/2021

5. Taarifa ya Idara ya Utawala na Rasilimali watu kwa mwezi Novemba, 2021

6. Kupokea na kujadili taarifa ya mapato na matumizi kwa mwezi Novemba, 2021

7. Taarifa Mbalimbali
    i. Taarifa ya mapokezi ya fedha kwa mwezi Novemba,, 2021
    ii. Mapendekezo ya kutumia 40% ya mapato ya ndani mwezi Novemba,, 2021
    iii. Ombi la kubadili matumizi ya Tsh. 20,000,000 kutoka katika mradi wa ulipaji wa fidia katika maeneo.
    iv. Taarifa ya Watumishi (siri)

8. Kufunga Kikao

## MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO CHA KUJADILI TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI MWEZI OKTOBA, 2021 KILICHOFANYIKA TAREHE 14/12/2021 KATIKA UKUMBI WA CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI SIKONGE (FDC)

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

| S.NA | JINA KAMILI | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Rashid M. Magope | Diwani Kaya Tutuo - Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Mayeka T. Mbusa | Diwani Kata ya Kilumbi - Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Ester P. Kayombi | Diwani V/Maalum -Mjumbe |
| 4. | Mhe. Omari R. Kategire | Diwani Kata ya Mkolye - Mjumbe |
| 5. | Mhe. Yusuph K. Ahmaed | Diwani Kata ya Kisanga - Mjumbe |
| 6. | Mhe. Juma B. Ikombola | Diwani Kata ya Misheni- Mumbe |
| 7. | Mhe. Amina S. Kaombwe | Diwani V/Maalum - Mjumbe |
| 8. | Mhe. Gastor L. Lwambano | Diwani Kata ya Kiloleli - Mjumbe |
| 9. | Mhe. Andrea P. Masanja | Diwani Kata ya Nyahua -Mjumbe |
| 10. | Mhe. Joseph G. Kakunda | Mbunge Jimbo la Sikonge - Mjumbe |

**WAJUMBE AMBAO HAWAKUHUDHURIA - HAKUNA**

**WATAALAM WALIOHUDHURIA**

| S.NA | JINA KAMILI | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1. | Ndg. Seleman M. Pandawe | Mkurugenzi Mtendaji (W) - Katibu |
| 2. | Ndg. Lenatus Mahimbali | Katibu Tawala (W) |
| 3. | Ndg. Nico A. Kayange | Mkuu wa Idara ya Utawala na Rasilimali Watu (W) |
| 4. | Ndg. Husen H. Mchomvu | Kaimu Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika (W) |
| 5. | Ndg. Gerald Mwagalazi | Kaimu Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi (W) |
| 6. | Ndg. Susana M. Makoye | Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi (W) |
| 7. | Ndg. Kassim Ismail | Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara (W) |
| 8. | Ndg. Yusuph Hamza | Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari (W) |
| 9. | Ndg. Aidan M. Frument | Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji (W) |
| 10. | Ndg. Tito E. Luchagula | Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii (W) |
| 11. | Ndg. Philipo N. Olotu | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi (W) |
| 12. | Ndg. Anna Kapama | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA (W) |
| 13. | Ndg. Pascal Kapiga | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sheria (W) |
| 14. | Ndg. Bwenge A. Mwesigwa | Kaimu Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira (W) |

| | | |
|---|---|---|
| 15. | Ndg. Shadrack T. Baruti | Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi (W) |
| 16. | Dr. Theopista Elisa | Kaimu Mkuu wa Idara ya Afya na Ustawi wa Jamii (W) |
| 17. | Ndg. Kelvin E. Msacky | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili (W) |
| 18. | Ndg. Bicko B. Mgeni | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi (W) |
| 19. | Ndg. Emmanuel M. Lufungulo | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani (W) |
| 20 | Ndg. Samwel John | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ufugaji Nyuki (W) |

**SEKRETARIETI**

| S.NA | JINA KAMILI | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1. | Ndg. Leonard Kapesula | Katibu wa Kamati |
| 2. | Ndg. Omari Masuha | Katibu wa Kamati Msaidizi |
| 3. | Ndg. Thadeo M. Revocatus | Katibu wa Kamati Msaidizi |
| 4. | Ndg. Pili A. Masaza | Katibu wa Kamati (H/W/Bunda) |

**Ajenda za kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha tarehe 14/12/2021**

1. Kufungua kikao.
2. Kuridhia ajenda.
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha tarehe 12/11/2021.
4. Yatokanayo na kikao cha tarehe 12/11/2021.
5. Taarifa ya Idara ya Utawala na Rasilinali Watu mwezi Oktoba, 2021.
6. Taarifa ya Mapato na Matumizi mwezi Oktoba, 2021.
7. Taarifa mbalimbali
   - i. Taarifa ya mapokezi ya fedha mwezi Oktoba, 2021.
   - ii. Mapendekezo ya matumizi ya asilimia 40 ya mapato ya ndani mwezi Oktoba, 2021.
   - iii. Mapendekezo ya gharama za madini ya ujenzi.
   - iv. Taratibu za usimamizi wa ujenzi wa majengo ya **EMD na ICU.**
8. Kufunga kikao.

**MUHTASARI NA. HWS/FUM/2021 - 2022/03/01 KUFUNGUA KIKAO.**

1.1 Katibu wakati akimkaribisha Mwenyekiti afungue kikao alisema kuwa tayari ameanza kuyafanyia kazi maelekezo mbalimbali ya wajumbe kuhusu masuala yafuatayo:-

1.1.1 **Ufanyikaji wa vikao kwa kuchelewa.**

Kuwa, tayari Menejimenti imeijadili changamoto hiyo katika vikao vyake hivyo aliahidi kufanya mabadiliko ili vikao/mikutano iwe inafanyika kwa kuzingatia kalenda ya vikao.

1.1.2 **Uboreshaji wa utendaji kazi kwa Sekretarieti ya vikao katika kuratibu vikao vya Halmashauri (kuandika majadiliano na maazimio wakati wa vikao, uandaaji wa Mihtasari pamoja na shughuli nyingine zinazohusiana na masuala ya vikao).**
Alisema kuwa ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) imeongeza nguvu katika ofisi ya Katibu wa Kamati kwa kumleta mtumishi mmoja kutoka Idara ya Elimu Sekondari ili asaidiane na Makatibu wa Kamati waliopo ikiwa ni pamoja na kumuomba Katibu wa Kamati kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Bunda ili awajengee uwezo Makatibu wa Kamati waliopo pamoja na kubadilishana uzoefu ambapo Katibu huyo atakuwepo katika Halmashauri hii kwa muda usiopungua siku tatu (03).

1.1.3 Baada ya maelezo hayo, alimkaribisha Mwenyekiti afungue kikao.

1.1.4 Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe wote kwenye kikao hicho.

1.1.5 Kabla hajafungua kikao alisema yafuatayo:-

1.1.6 Alimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwajaalia wajumbe wote na wataalam afya njema iliyowawezesha kuhudhuria kikao hicho.

1.1.7 Alisema kuwa kikao hicho ni cha kawaida kwa mujibu wa ratiba ya vikao vya Halmashauri.

1.1.8 Alizungumzia suala la ucheleweshaji wa vikao ambapo alisema kuwa tayari Menejimenti imeanza kulifanyia kazi kwa mujibu wa maelezo ya Mkurugenzi Mtendaji (W) hivyo ni matarajio yake kuwa vikao vyote vya kisheria vitafanyika kwa wakati.

1.1.9 Aliwataka wajumbe wanapokuwa kikaoni wazingatie maelekezo mbalimbali waliyoyapata katika semina ya kuwajengea uwezo iliyofanyika kwa muda wa siku mbili kuanzia tarehe 19 – 20/11/2021.

1.1.10 Alizungumzia suala la uboreshaji wa mapato pamoja na uibuaji wa vyanzo vipya vya mapato.

1.2.5 Alifungua kikao saa 05:01asubuhi.

1.3 Baada ya Mwenyekiti kufungua kikao, aliwataka watumishi wageni waweze kujitambulisha mbele ya wajumbe ili wapate kufahamiana ambapo Bi. Pili A. Masaza alisema kuwa yeye ni Katibu wa Kamati akitokea katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda iliyopo mkoani Mara lakini pia Bw. Thadeo M. Revocatus alisema kuwa yeye ni mwalimu akitokea katika Shule ya Sekondari Ugunda ambaye kwa sasa anafanya kazi kama Katibu wa Kamati katika Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge.

**MUHTASARI NA. HWS/FUM/2021 - 2022/03/02 KURIDHIA AJENDA**

2.1 Ajenda nane (8) ziliwasilishwa kwenye kikao.

2.2 Wajumbe walizipokea ajenda zote nane (8) kuwa zijadiliwe kwenye kikao hicho.

**MUHTASARI NA. HWS/FUM/2021 - 2022/03/03 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 12/11/2021**

3.1 Muhtasari huo ulisomwa kwenye kikao.

3.2 Wajumbe waliupokea Muhtasari huo.

3.3 Mwenyekiti na Katibu waliweka saini na kuwa kumbukumbu sahihi za kikao baada ya kufanya masahihisho yafuatayo:-

3.3.1 Uk. Na. 8 Sentensi yenye Namba za kirumi **vi** badala ya kusomeka Elimu Msingi Isomeke Elimu Sekondari

3.3.2 Uk. Na. 8 Sentensi yenye Namba za Kirumi **viii** iondolewe kwa kuwa ilijirudia yaani ilifanana na sentensi yenye Namba za Kirumi **i**.

**MUHTASARI NA. HWS/FUM/2021 - 2022/03/04 YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 12/11/2021.**

4.1 Utekelezaji wa yatokanayo na kikao hicho uliwasilishwa kwenye kikao.

4.2 Wajumbe waliupokea utekelezaji huo na kuujadili.

4.3 **MAJADILIANO.**

4.3.1Kuhusu azimio Na.1 la MuhtasariNa. 2/KAMFUM/2021/2022/4 lililohusu fedha Tsh. 4,000,000.00 iliyotengwa kwa ajili ya ujenzi wa choo cha wanafunzi katika shule ya Msingi Kiloleli ipelekwe mapema na taarifa ya utekelezaji iwasilishwe kwenye kikao. Azimio hilo lilitekelezwa na Mkurugenzi Mtendaji (W) kwa maelezo kuwa changamoto hiyo ilitokana na tatizo la kimfumo hata hivyo tayari imetatuliwa na fedha kiasi cha Tsh, 4,000,000.00 zilikwishaingizwa kwenye Akaunti ya shule ya Msingi Kiloleli na Mwalimu Mkuu wa shule hiyo amethibitisha kupokea fedha hizo.

4.3.1.1Wajumbe waliupokea utekelezaji huo, waliujadili na kufunga hoja.

4.3.2 Kuhusu azimio Na. 2 la MuhtasariNa. 2/KAMFUM/2021/2022/4 lililohusu kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Menejimenti kufuatia mapendekezo yaliyotolewa na Mkaguzi wa Ndani wakati wa ukaguzi maalum katika ujenzi wa mradi wa wodi 3 katika Hospitali ya Wilaya. Azimio hilo lilitekelezwa na Mkurugenzi Mtendaji (W) kwa kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa hoja za ukaguzi maalum katika ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Sikonge.

4.3.2.1 Wajumbe waliupokea utekelezaji huo, waliujadili kwa kupitia hoja moja baada ya nyingine na mwisho walitoa mapendekezo yao kwa kila hoja kama inavyosomeka katika jedwali hapa chini:-

| S.Na | HOJA | MAONI YA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO |
|---|---|---|
| 1 | Hoja Na. 5.2. inayohusu fedha zilizotumika kulipa vifaa vya ujenzi Tsh. | - Kamati imeridhia mapendekezo ya Mkaguzi wa Ndani. |

| | | |
|---|---|---|
| | 450,992,580.09 | - Mkurugenzi Mtendaji (W) abainishe vifaa vyote vilivyobaki kwa idadi na thamani yake ikiwa ni pamoja na kuvibadilisha kuwa fedha katika miradi mingine ya afya inayoendelea kutekelezwa /yenye mahitaji na fedha zitakazopatikana ziingizwe kwenye Akaunti husika kwa ajili ya kuendelea kutekeleza mradi wa Hospitali.<br>- Menejimenti ihakikishe kuwa Makisio ya Ujenzi (BOQ) yanayoandaliwa ya akisi mahitaji halisi ya miradi |
| 2 | Hoja Na. 5.2.4 inayohusu jumla ya malipo ya mafundi kwa Akaunti zote kwa kulinganisha na mikataba yao ni Tsh. 50,540,800.00 kati ya mikataba ya Tsh. 76,603,000.00 | - Kamati imeridhia utekelezaji wa Menejimenti<br>- Menejimenti ihakikishe kuwa, malipo ya mafundi yanalipwa kwa wakati |
| 3 | Hoja Na. 5.4 inayohusu madeni ambayo hayajalipwa kwa Wazabuni kwa kazi ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ni Tsh. 52.263,200.00 | - Kamati imeridhia utekelezaji wa Menejimenti |
| 4 | Hoja Na. 5.5 inayohusu usimamizi usioridhisha katika ujazaji wa vifaa kwenye leja | - Kamati imeridhia utekelezaji wa Menejimenti hasa katika kipengele kilichotamka kuwa, "Menejimenti itaboresha ili msimamizi wa mradi asiwe Katibu wa Mapokezi na Utunzaji"<br>- Kamati za Mapokezi ziwe zinajengewa uwezo ili zitambue wajibu na mipaka yao kiutendaji. |
| 5 | Hoja Na. 5.6 inayohusu vifaa vilivyokopwa kutoka kwenye ujenzi wa Wodi tatu na havijarejeshwa. | - Menejimenti ihakikishe kuwa vifaa vyote vilivyoazimwa vinarejeshwa kwa wakati.<br>- Kamati imepiga marufuku suala la kuazimana vifaa kutoka mradi mmoja kwenda mwingine kwani hali hiyo husababisha miradi iliyoazimwa vifaa vyake kushindwa kukamilika kwa wakati. |
| 6 | Hoja Na. 5.7 inayohusu vifaa vilivyopokelewa kutoka miradi mingine na kwa wazabuni bila maelezo ya msingi na namna wazabuni watakavyolipwa Tsh. 5,140,407.40 | - Kamati imeridhia utekelezaji wa Menejimenti |
| 7 | Hoja Na. 5.8 inayohusu vifaa vilivyosalia na thamani yake | - Kamati imeridhia utekelezaji wa Menejimenti |
| 8 | Hoja Na. 5.9 inayohusu gharama za vifaa vya kukamilisha shughuli zilizobaki Tsh. 72,341,000.00 | - Kamati imeridhia utekelezaji wa Menejimenti |

| | | |
|---|---|---|
| 9 | Hoja Na. 5.10 inayohusu makato ya kodi ya zuio ambayo hayajawasilishwa TRA Tsh. 3,110,891.98 | - Kamati imeridhia utekelezaji wa Menejimenti |
| 10 | Hoja Na. 5.11 inayohusu malipo ambayo hayakuambatisshwa lisiti za kieletroniki ( EFD RIST) Tsh. 167,555,064.00 | - Kamati imeridhia mapendekezo ya Mkaguzi wa Ndani.<br>- Mkurugenzi Mtendaji (W) amtake Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani (W) afanye uhakiki wa stakabadhi za kielektroniki zenye thamani ya Tsh. 167,555,064.00 ili ajiridhishe na uhalali wake na akiridhika aweze kufunga hoja. |
| 11 | Hoja Na. 5.12 inayohusu malipo ya manunuzi ya vifaa vyenye mapungufu mbalimbali na kutoingizwa kwenye leja kikamilifu Tsh. 161,845,548.89 | - Kamati imeridhia utekelezaji wa Menejimenti |
| 12 | Hoja Na. 5.13 inayohusu malipo ya manunuzi ya vifaa yaliyofanyika zaidi kwa wazabuni katika ujenzi wa wodi tatu (03) za Hospitali ya Wilaya Tsh. 962,000.00 | - Mkurugenzi Mtendaji (W) amtake Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani (W) afanye uhakiki wa lisiti Na. 41752122427 ya tarehe 04/11/2021 ili ajiridhishe na urejeshaji wa fedha zilizolipwa zaidi kwa wazabuni kwenye malipo ya ununuzi ya vifaa katika ujenzi wa wodi tatu (03) na akiridhika aweze kufunga hoja. |
| 13 | Hija Na. 5.14 inayohusu hali ya utekelezaji wa mradi (wodi tatu (03). | - Kamati imeridhia utekelezaji wa Menejimnetii.<br>- Mkurugenzi Mtendaji afanye uchunguzi kubaini wale wote waliohusika kupendekeza eneo la ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ambalo lipo mbugani hivyo kusababisha mradi huo kushindwa kukamilika kwa wakati kutokana na kuongezeka kwa gharama za ujenzi.<br>- Aidha utekelezaji wa agizo hilo uwasilishwe kwenye kikao cha Kamati cha robo ya II 2021/2022. |

**MUHTASARI NA. HWS/FUM/2021 - 2022/03/05 TAARIFA YA IDARA YA UTAWALA NA RASILIMALI WATU MWEZI OKTOBA, 2021**

5.1Taarifa hiyo iliwasilishwa kwenye kikao na Mkuu wa Idara ya Utawala na Rasilimali Watu (W) kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji (W) kuwa,

Ikama ya watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge 2021/2022

| Idara/Vitengo | Ikama | Waliopo | Upungufu |
|---|---|---|---|
| 18 | 2,519 | 1,662 | 857 |

5.1.1 Aidha katika kipindi cha mwezi Oktoba, 2021 Idara ya Utawala na Rasilimali Watu iliweza kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Usimamiaji wa ufanyikaji wa vikao mbalimbali vya Kisheria vikiwemo vikao vya Serikali za Vijiji (VDC), Vikao vya Maendeleo ya Kata (WDC), Mikutano ya hadhara ya Vijiji, vikao vya kisheria na mikutano ya ngazi ya Halmashauri. Hivyo Vijiji vilivyofanya vikao vya Serikali za Vijiji kwa mwezi husika ni Vijiji 14, mikutano ya hadhara kwa robo ya I 2021/2022 ni mikutano 21 na Kamati za Maendeleo za Kata, vikao 14.

(ii) Kushughulikia maslahi ya Wahe. Madiwani yakiwemo posho za madaraka kwa Wenyeviti wa Kamati za kudumu za Halmashauri wapatao wa tano (05) zilizogharimu jumla ya Tsh. 1, 150,000.00, posho za mwezi kwa Wahe. Madiwani Tsh. 9,500,000.00 na makato ya Bima ya Afya Tsh. 285,000/= ambayo ni asilimia 03 ya Mwajiri.

5.1.2 Aidha changamoto zinazokabili Idara hiyo pamoja na njia za utatuzi wa changamoto hizo zilibainishwa.

5.2 Wajumbe waliipokea taarifa hiyo, waliijadili na kusema kuwa, kuna wimbi kubwa la watumishi wanaotaka kuhama katika Halmashauri hii kutokana na sababu mbalimbali. Kwa mantiki hiyo wajumbe waliona kuna haja ya Halmashauri kutafuta kila namna kuhakikisha watumishi hao wanaendelea kubaki katika Halmashauri hii.

5.2.1 Hata hivyo walipendekeza njia mbalimbali ambazo zinaweza kuwafanya watumishi hao kuendelea kubaki katika Halmashauri hii zikiwemo:-

1. Kuwapa watumishi mikopo kama motisha.
2. Mwenyekiti wa Halmashauri kukaa na kuzungumza na watumishi hao ili kubaini changamoto zinazowakabili.
3. Kuimarisha utawala bora.

5.2.2 Kuhusu suala la ufanyikaji wa vikao kwa wakati katika ngazi za Kata na Vijiji pamoja na uratibu wa mihtasari inayopokelewa katika masijala ya wazi kutoka ngazi hizo za Kata na Vijiji, kikao kilitoa ushauri.

5.2.2.1 **USHAURI.** Mkurugenzi Mtendaji (W) ahakikishe anapeleka na kusimamia kalenda ya vikao ili vikao vya Ngazi ya Kata na Vijiji viweze kufanyika kwa kuzingatia kalenda hiyo.

5.2.2.2 **USHAURI.**Mkurugenzi Mtendaji (W) ahakikishe kuwa mihtasari inayopokelewa katika masijala ya wazi kutoka ngazi ya Kata na Vijiji inaratibiwa vizuri (upokeaji pamoja na utanzaji wake).

**MUHTASARI NA. HWS/FUM/2021 - 2022/03/06 TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI MWEZI OKTOBA, 2021**

6.1 Taarifa hiyo iliwasilishwa kwenye kikao na Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara (W) kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji (W).

6.2 Wajumbe waliipokea taarifa hiyo, waliijadili na kuipitisha kama ifuatavyo:-

**Muhtasari wa taarifa ya mapato na matumizi mwezi Julai 2021 - Oktoba, 2021**

**A. TAARIFA YA MAPATO**

| NA. | MAELEZO YA MAPATO | MAKISIO NA BAKAA | MAPATO HALISI YA OKTOBA | JULAI 2021 - OKTOBA, 2021 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|
| I | Mapato kutokana na vyanzo vya ndani | 3,229,000,000 | 288,685,123 | 1,051,425,269 | 33 |
| II | Mapato ya Mishahara | 14,894,666,000 | 1,247,741,050 | 5,001,794,650 | 33.6 |
| III | Mapato ya Matumizi Mengineyo | 812,315,000 | 23,482,333 | 232,289,332 | 28.6 |
| IV | Ruzuku za Miradi | 9,339,276,000 | 2,898,345,556.26 | 4,018,967,224 | 43 |
| | **JUMLA** | **27,115,257,000** | 4,458,254,062.26 | 10,304,476,475 | 38 |

**B. TAARIFA YA MATUMIZI.**

| NA. | MAELEZO YA MATUMIZI | MAKISIO NA BAKAA | MATUMIZI HALISI YA OKTOBA | JULAI 2021 - OKTOBA, 2021 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|
| I | Matumizi kutokana na vyanzo vya ndani | 2,069,000,000 | 201,565,919.83 | 507,620,390.43 | 24.5 |
| II | Matumizi ya Mishahara | 14,894,666,000 | 1,247,741,050 | 5,001,794,650 | 33.6 |
| III | Matumizi Mengineyo | 812,315,000 | 8,725,900.00 | 259,524,739.26 | 31.9 |
| IV | Ruzuku za Miradi | 9,339,276,000 | 545,825,644.27 | 911,711,325.85 | 9.8 |
| | **JUMLA** | **27,115,257,000** | 2,003,858,514.1 | 6,680,651,105.54 | 24.6 |

6.3 Wajumbe walijadili kwa kina kuhusu suala la ukusanyaji wa mapato ambapo walisema kuwa bado matumizi ya fedha mbichi yaani fedha ambazo hazijapelekwa Benki kutoka kwa wakusanyaji wa mapato yanaendelea licha ya katazo la kutotumia fedha mbichi kutolewa katika vikao vilivyopita. Katika majadiliano wajumbe walimtuhumu Mhasibu wa Maputo (W) kuwa amekuwa akiagiza fedha kutoka kwa wakusanyaji wa mapato na kuzitumia kabla hazijapelekwa Benki.

6.3.1 Kutokana na tuhuma hizo, kikao kilijadili na kuamua iundwe Timu kwa ajili ya uchunguzi wa tuhuma hiyo na kuwasilisha taarifa ya uchunguzi katika kikao.

6.3.2 **AZIMIO.** Mkurugenzi Mtendaji (W) aunde timu ya Wataalam kwa ajili ya kufanya uchunguzi kwa lengo la kujiridhisha na tuhuma kuhusu Mhasibu wa Mapato (W) kuchukua na kutumia fedha mbichi/fedha ambazo hazijapelekwa Benki kutoka kwa Wakusanyaji wa mapato.

6.4 Aidha wajumbe walitaka kufahamu mwenendo wa ukusanyaji wa mapato na upelekaji wa fedha Benki hivyo walitaka kupata takwimu za wakusanyaji wote wa mapato.

6.4.1 **AZIMIO**.Mkurugenzi Mtendaji (W) awasilishe katika kikao kijacho taarifa ya wakusanyaji wa mapato kwa kuonesha Wakusanyaji waliobenki fedha za makusanyo na ambao hawajabenki/walioning'iniza. Hata hivyo wajumbe walisistiza kuhusu Wakusanyaji wa mapato kulipwa stahiki zao kwa wakati.

**MUHTASARI NA. HWS/FUM/2021 - 2022/03/07 TAARIFA MBALIMBALI**

7.1**Taarifa ya mapokezi ya fedha mwezi Oktoba, 2021.**

7.1.1 Taarifa hiyo iliwasilishwa kwenye kikao na Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara (W) kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji (W) kuwa, Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge ilipokea fedha mbalimbali kama ifuatavyo:-

a. Ruzuku ya matumizi mengineyo na posho ya wito wa dharura Tsh. 23,482,333.33.
b. Ruzuku ya mishahara kwa watumishi Tsh. 1,244,236,050.
c. Elimu bila malipo Tsh. 80,739,866.64 ikiwa Elimu Msingi Tsh. 57,291,612.03 na Elimu Sekondari Tsh. 23,448, 254.61.
d. Posho za Madiwani Tsh. 9,500,000.00.
e. Ruzuku kutoka RDF Tsh. 21.653,414.62.
f. Ruzuku kwa ajili ya uendeshaji wa mitihani Tsh. 467,913,900 ikiwa mtihani wa darasa la nneTsh. 172,011,400, Kidato cha Pili Tsh 116,532,500 na kidato cha Nne Tsh. 179,370,000.00.
g. Ruzuku kwa ajili ya ujenzi wa madarasa shule za Msingi na Sekondari ( Mradi wa COVID 19 ) Tsh. 1,960,000,000.00 ikiwa Tsh. 780,000,0000 kwa ajili ya shule za Msingi na Tsh. 1,180,000,000. 00 kwa ajili ya shule za sekondari.
h. Ruzuku kwa ajili ya ujenzi wa madarasa - Elimu ya Sekondari Tsh. 112,500,000.00

7.1.2 Wajumbe waliipokea taarifa hiyo, waliijadili na kuipitisha.

7.1.3 **Mapendekezo ya kutumia asilimia 40 ya mapato ya ndani kwa mwezi Oktoba, 2021.**

7.2.1 Taarifa hiyo iliwasilishwa kwenye kikao na Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji (W) kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji (W) kuwa, katika mwezi Oktoba, 2021 Menejimenti iliweza kuhamisha jumla ya Tsh. 85,000,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali. Hivyo aliwaomba wajumbe waridhie kiasi hicho cha fedha kwenda kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Mikopo ya vikundi vya Wanawake Vijana na Walemavu Tsh. 30,000.000.00.
(ii) Kuwezesha upembuzi yakinifu (Feasibility Study) katika mradi wa umwagiliaji wa Kalupale Tsh. 150,160,000.00.

(iii)Ununuzi wa Madirisha ya Alminium katika shule ya Sekondari Mpombwe Tsh. 3.840,000.00 ili kutekeleza agizo la Mkuu wa Mkoa wa Tabora aliyefanya ziara wilayani Sikonge tarehe 03/12/2021.

Jumla Tsh. 85,000,000.00

7.2.2 Wajumbe waliipokea taarifa hiyo, waliijadili na kuridhia jumla ya Tsh. 85,000,000.00 ziweze kutekeleza shughuli tajwa hapo juu. Aidha waliisisitiza Menejimenti ihakikishe inatoa mikopo kwenye vikundi vyenye tija/miradi mikubwa tu kama maelekezo ya Serikali yalivyotolewa.

7.3 **Mapendekezo ya gharama za madini ya ujenzi.**

7.3.1 Taarifa hiyo iliwasilishwa kwenye kikao na Kaimu Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira (W) kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji (W) kuwa, mnamo tarehe 02/12/2021, Mkuu wa Wilaya ya Sikonge alifanya kikao na Wakandarasi wa barabara za Sikonge, Mkurugenzi Mtendaji (W), Mkuu wa Idara Fedha na Biashara (W) pamoja na Kaimu Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira.

7.3.1.1 Mkuu huyo wa Wilaya aliitisha kikao hicho baada ya kupokea maombi ya Wakandarasi ya kupunguziwa tozo ya ushuru wa madini ya ujenzi kwa maelezo kuwa katika mikataba yao hawakuainisha kipengele hicho.

7.3.1.2 Aidha gharama za ushuru wa madini ya ujenzi kama zilivyoainishwa katika Sheria ndogo ya Halmashauri kwa tangazo la Serikali Na. 574 la tarehe 18/12/2015 ni kama ifuatavyo:-

| Na | Aina ya madini | Ujazo | Gharama |
|---|---|---|---|
| 1 | Changarawe | Tnai 7 | 5000/= tripu |
| 2 | Udongo | Tnai 7 | 3000/= tripu |
| 3 | Kokoto | Tnai 7 | 5000/= tripu |
| 4 | Mchanga | Tnai 7 | 3000/= tripu |
| 5 | Udongo wa tofali | Tnai 7 | 3000/= tripu |

7.3.1.2Kutokana na ombi hilo la Wakandarasi, Menejimenti ilieleza kuwa mchakato na utekelezaji wa Sheria huwa unafuata ngazi mbalimbali mpaka Sheria hiyo ianze kutumika.Hivyo kubadili Sheria kunahitaji michakato hiyohiyo kama ilivyo tungwa na kukubaliwa kutumika kutokana na Sheria mama ambayo ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

7.3.1.3 Kwa mantiki hiyo walishauri mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria yafuate mchakato wa ubadilishaji/urekebishaji wa Sheria.

7.3.2 Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kusema kuwa, kwa kuwa ushuru huo haukuwa ukikusanywa licha ya kuwepo kwa Sheria hiyo na kwa kuwa tayari Wakandarasi hao wapo tayari kulipa suhuru huo kwa kupunguziwa gharama za tozo kwa sababu kwenye mikataba yao hawakuwa na kipengele hicho, walishauri kuwa Wakandarasi hao waandike barua za maombi ya kupunguziwa tozo hiyo ya ushuru wa madini ya ujenzi

na kuwa taarifa hiyo itajadiliwa kwa kina na kutolewa maamuzi baada ya maombi hayo kuwa yamewasilishwa katika ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W).

7.4 **Taratibu za usimamizi wa ujenzi wa majengo ya EMD na ICU.**

7.4.1 Taarifa hiyo iliwasilishwa kwenye kikao na Kaimu Mkuu wa Idara ya Afya na Ustawi wa Jamii (W) kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji (W) kuwa, Serikali kupitia fedha za mpango maalum wa ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVICO 19 imetenga Tsh. Bilioni 236 kwa ajili ya kupeleka katika maeneo yafuatayo:-

(i) Ujenzi wa majengo ya huduma za wagonjwa wa dharura na ununuzi wa vifaa.
(ii) Ujenzi wa majengo 26 ya ICU pamoja na ununuzi wa vifaa tiba.
(iii)Ujenzi wa nyumba za watumishi 150.
(iv)Kuimarisha huduma za Tiba hewa, mitambo 6 ya kuzalisha Oxygen inatarajiwa kununuliwa.
(v) Kuimarisha huduma za ugunduzi na utambuzi wa magonjwa, ununuzi wa X - Ray za kidigitali na vifaa tiba mbalimbali.
(vii) Kuweka mfumo imara wa rufaa ya ununuzi wa magari ya wagonjwa 195, ununuzi wa magari 112 ya usimamizi na ufuatiliaji, ununuzi wa vifaa tiba kama vita X - Ray za kidigitali ambazo zitasambazwa katika Halmashauri zote nchini

7.4.2 Pamoja na mambo mengine muhimu yaliyooneshwa kwenye taarifa hiyo, taarifa ilionesha pia, Faida za kuwa na majengo ya huduma za dharura na majengo ya kuhudumia wagonjwa mahututi, changamoto tarajiwa baada ya majengo hayo kukamilika, mambo ya kuzingatia wakati wa utekelezaji wa miradi, muonekano wa jengo la EMD na matumizi yake, Ujenzi wa nyumba ya watumishi ambapo nyumba hiyo itachukua familia tatu itajengwa katika eneo la Hospitali ya Wilaya, uongozi na utawala wa Kitengo cha EMD katika Hospitali ya Wilaya, Kuwajengea uwezo watumishi watakaohudumu katika jengo la EMD, muendelezo wa huduma pamoja na mtiririko wa wagonjwa katika Kitengo cha EMD.

7.4.3 Wajumbe waliipokea taarifa hiyo, waliijadili na kuipitisha.

7.5 **Nasaha kutoka kwa viongozi.**

7.5.1 **Nasaha kutoka kwa Katibu Tawala (W).**

7.5.1.1 Aliwataka wajumbe watumie kauli za staha wakati wa majadiliano kwenye vikao na mikutano ya kisheria.

7.5.1.2 Aliwataka Wataalam pia kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu na uaminifu.

7.5.2 **Nasaha kutoka kwa Mbunge (Jimbo la Sikonge)**

7.5.2.1 Alimshukuru Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuongeza muda wa kukabidhi majengo ya COVID 19 hivyo alimtaka Mkurugenzi Mtendaji Wilaya kuhakikisha kuwa kufikia tarehe 31/12/2021 majengo yote yawe yamekamilika.

7.5.2.2 Alizungumzia suala la utawala bora hivyo alishauri kuwa si vizuri kila mara makalipio yakafanyika kwa maandishi kwani kalipio linaweza kutolewa hata kwa mdomo tu na Mtumishi/Watumishi wakabadili mienendo yao.

7.5.2.3 Alisisitiza mbinu mbalimbali zitumikekuhakikisha watumishi wanaendelea kubaki katika Halmashauri hii na siyo kufikiri kuhama kutokana na hali ya upungufu wa watumishi iliyopo.

**MUHTASARI NA. HWS/FUM/2021 - 2022/03/08 KUFUNGA KIKAO.**

8.1 Katibu alimkaribisha Mwenyekiti afunge kikao.

8.2 Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe wote kwa mchango wa mawazo waliotoa.

8.2.1 Aliitaka Menejimenti kutekeleza yale yaote yaliyoshauriwa na kuazimiwa na wajumbe.

8.2.2 Alisisitiza matumizi ya lugha za staha kwa wajumbe wakati wa majadiliano.

8.2.3 Alisema kuwa kama taratibu zinaruhusu wakusanyaji wa mapato wawe wanabenki makusanyo yao kila siku au baada ya siku moja hasa kwa wale ambao wapo kwenye maeneo ambayo huduma za kibenki zinapatikana kwa urahisi.

8.2.4 Alifunga kikao saa 12:14 jioni.

**UMETHIBITISHWA.**

**SAINI YA MWENYEKITI**.......................................**SAINI YA KATIBU**.........................

**JINA LA MWENYEKITI** MAYURA .T. MBUSA **JINA LA KATIBU**.........................

**TAREHE** 17/12/2021

## AYATOKANAYO NA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO CHA TAREHE 14/12/2021

| Na. | AZIMIO | | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| 1. | Mkurugenzi Mtendaji (W) abainishe vifaa vyote vilivyobaki kwa idadi na thamani yake ikiwa ni pamoja na kuvibadilisha kuwa fedha katika miradi mingine ya afya inayoendelea kutekelezwa /yenye mahitaji na fedha zitakazopatikana ziingizwe kwenye Akaunti husika kwa ajili ya kuendelea kutekeleza mradi wa Hospitali. | | Agizo limezingatiwa, utekelezaji unaendelea kufanyika majibu ya utekelezaji yatatolewa katika kikao cha robo ya pili mwaka wa fedha 2021/2022 |
| 2 | Mkurugenzi Mtendaji (W) amtake Mkaguzi wa Ndani kufanya uhakiki wa stakabadhi za kielektroniki zenye thamani ya Tsh. 167,555,064.00 ili ajiridhishe na uhalali wake na akiridhika aweze kufunga hoja. | | Agizo limezingatiwa majibu ya utekelezaji yatatolewa kikao kijacho katika robo ya pili 2021/2022. |
| 3 | Mkurugenzi Mtendaji (W) amtake Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani (W) fanye uhakiki wa lisiti Na. 41752122427 ya tarehe 04/11/2021 ili ajiridhishe na urejeshaji wa fedha zilizolipwa zaidi kwa wazabuni kwenye malipo ya ununuzi ya vifaa katika ujenzi wa wodi tatu (03) na akiridhika aweze kufunga hoja. | | Agizo limezingatiwa majibu ya utekelezaji yatatolewa kikao kijacho katika robo ya pili 2021/2022. |
| 4 | Mkurugenzi Mtendaji afanye uchunguzi kubaini wale wote waliohusika kupendekeza eneo la ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ambalo lipo mbugani hivyo kusababisha mradi huo kushindwa kukamilika kwa wakati kutokana na kuongezeka kwa gharama za ujenzi.<br>Aidha utekelezaji wa agizo hilo uwasilishwe kwenye kikao cha robo ya II 2021/2022. | | Agizo limezingatiwa majibu ya utekelezaji yatatolewa kikao kijacho katika robo ya pili 2021/2022. |
| 5 | Mkurugenzi Mtendaji (W) aunde timu ya Wataalam kwa ajili ya kufanya uchunguzi kwa lengo la kujiridhisha na tuhuma kuhusu Mhasibu wa Mapato (W) kuchukua na kutumia fedha mbichi/fedha ambazo hazijapelekwa Benki kutoka kwa Wakusanyaji wa mapato. | | Barua ya uteuzi wa wajumbe wa timu ya uchunguzi imeandikwa na kupatiwa wahusika kwa lengo la kutekeleza agizo la kikao. |
| 6 | Mkurugenzi Mtendaji (W) awasilishe katika kikao kijacho taarifa ya wakusanyaji wa mapato kwa kuonesha Wakusanyaji waliobenki fedha za makusanyo na ambao hawajabenki/walioning'iniza. Hata hivyo wajumbe walisistiza kuhusu Wakusanyaji wa mapato kulipwa stahiki zao kwa wakati. | | Azimio limezingatiwa ili kuhakikisha wakusanya mapato wanalipa kwa wakati, Halmashauri imeshawalipa hadi mwezi Novemba, 2021.<br>Hata hivyo taarifa ya fedha za makusanyo ambayo hayajabenkiwa/walioning'iniza itatolewa kwenye kikao. |